



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS



TAWALA LA MIKOANI NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI

MKOANI WA KILIMANJARO

Simu : 27-29 74369

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji

Wilaya,

S.I.P. 27,

Fax : 27- 29 74368

HAI.

Email: ded@haidc.go.tz

Tarehe : 03/06/2022

Kumb NA LG/ 2021/2022.

TANGAZO

**TANGAZO LA KUMPATA FUNDI (LOCAL FUNDI) KWA
AJILI YA UJENZI WA JENGU LA WODI YA WAZAZI
(MATERNITY), JENGU LA UPASUAJI (THEATRE), JENGU
LA KUFULIA(LAUNDRY) NA NJIA ZA KUPITISHA
WAGONJWA(WALK WAYS) KATIKA KITUO CHA AFYA
CHEKI MAJI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai kupitia Kituo cha Afya Cheki Maji anategemea kuanza ujenzi wa Jengo la Wodi ya Wazazi (Maternity), Jengo la Upasuaji (Theatre), Jengo la Kufulia (Loundry) na Njia za kupitisha wagonjwa (walk Ways) katika Kituo cha Afya Cheki Maji Wilaya ya Hai.

Hivyo napenda kutangaza kazi hii kwa mafundi wote wenye uwezo wa kujenga majengo ya serikali wajitokeze na kuomba kazi hii.

Mafundi wenye sifa na uzoefu wanatakiwa kuja kuchukua somu maalumu (schedule of labour) dondo shindani katika ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi Halmashauri ya Wilaya ya Hai.

Sifa za Mwombaji.

1. Awe ni raia wa Tanzania mwemeyuelewa mzuri wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza
2. Awe na umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea.
3. Awe na uelewa mzuri wa usalama na Afya awapo eneo la kazi.
4. Awe na timu ya kutosha ya mafundi mbalimbali kwa muda wote wa kazi mafundi mwashi, fundi bomba, fundi umeme, fundi carpenta nk.
5. Awemna uwezo wa kuandaa na kutekeleza mpango kazi wa mradi /miradi na kumaliza kwa wakati.

6. Awe mwadilifu na mwaminifu.
7. Uwezo wa kusimamia mafundi wenzake na vibarua.
8. Mwenye zana zote muhimu za kazi (tools).
9. Ada ya maombi ya kazi ya ufundi ni shilingi elfu ishirini (20,000/=) ikwa kila Jengo na fedha hii haitarudishwa.

Uzoefu.

1. Uzoefu wa kuanzia miaka mitano na kuendelea katika kazi ya ujenzi.
2. Awe amefanya kazi yoyote ya ujenzi /ukarabati wa majengo ya serikali walau miradi mitatu na hati ya huduma (certificate of service) au mikataba ya miradi iliyotekelizwa ambayo inafikika kwa udhibitisho(ambatanisha udhibitisho).
3. Awe na uwezo wa kusoma na kutafsiri mchoro/michoro ya majengo kwa lugha ya kiufundi.

Fomu za maombi ya kazi hii zinapatikana ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha manunuzi na ugavi na baada ya fomu kujazwa ziwekwe katika bahasha iliyofungwa vizuri na kuandikwa anuani ifuatayo , Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya
Hai.S.L.P 27 Hai.

Mwisho wa kupokea maombi haya ni 4:00 asubuh tarehe 09/06/2022 sehemu ya kuwasilisha maombi hayo ni ofisi ya Manunuzi na Ugavi Wilaya ya Hai S.L.P 27 . Ufunguzi wa maombi hayo utafanyika tarehe 09/06/2022 katika Ukumbi wa Halmashauri mbele ya waombaji watakaopenda kuhudhuria ufunguzi huo.

ANGALIZO: Fundi anatakiwa kuandika barua ya maombi ya kazi hii na kujaza fomu ya maombi kwa kupitia mchoro wa jengo/husika.

Limetolewa na

Dionis M. Myinga

Mkurugenzi Mtendaji (W)

HALMASHAURI YA WILAYA-HAI.

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
HAI



Sensa kwa maendeleo, jiandae kuhesabiwa Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022